# UJE ROHO MUUMBAJI

Polepole &
Kwa Uchaji

*Priestly Ordination of Deacon James Turuka*

Frt.Stanslaus B.Komba
Peramiho M.Seminary
April 2025.0696618932




2.Unaitwa mfariji, paji la Mwenyezi Mungu, chanzo cha uzima moto, pendo mpako wa Rohoni.

3.Mtoa wa vipaji saba, na kidole chake Mungu, Mwahidiwa naye Baba, na msemesha ndimi zetu.

4.Tia nuru akilini, na upendo mioyoni,Tegemeza miili yetu, kwa imara ya kudumu.

5.Ufukuze mashetani, na amani tupe hima, Hivyo uwe kiongozi, tuepuke ovu lote.

6.Umjulishe kwetu Baba,tukamjue pia Mwana, Tukakusadiki wewe, Roho utokaye kwao.

7.Atukuzwe Mungu Baba, na Mwanawe Mfufuka, Pia Roho Mtakatifu, kwa milele na milele.

AMINA. (ALELUYA).